# AZIMIO LA TABORA

## Juu ya Siasa ya Ujamaa wa KiDemokrasia

Juni 2015

# AZIMIO LA TABORA[1]

## Juu ya Siasa ya Ujamaa wa KiDemokrasia

**Limetolewa na**

**HALMASHAURI KUU YA CHAMA CHA ACT - WAZALENDO**

**Juni 2015**

1 Linalohuisha Azimio la Arusha lililotolewa na Chama cha TANU mnamo mwezi Februari mwaka 1967 na kutangaza rasmi siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

## NDOTO YETU YA TANZANIA NI

Taifa lenye kujitegemea kiuchumi na kiutamaduni, na ambalo linalinda na kudumisha usawa, ustawi wa jamii, uwajibikaji, demokrasia, na uongozi bora.

# YALIYOMO


**DIBAJI ........................................ i**

**SEHEMU YA KWANZA ........................... 1**

*1.1 Itikadi, Falsafa, Misingi na Madhumuni ya ACT-Wazalendo ........................... 1*

**SEHEMU YA PILI ............................ 13**

*2.1 Siasa ya Ujamaa wa kidemokrasia na ndoto ya Tanzania ............................. 13*

**SEHEMU YA TATU ............................ 17**

*3.1 Hali ya nchi na Matamko ya kisera .... 17*

*3.1.1 Kumomonyoka kwa umoja na kukithiri kwa rushwa na umaskini ............... 17*

*3.1.2 Mfumo wa uchumi unaonyonya wana vijijini........................................ 19*

*3.1.3 Tusisahau jambo hili, Azimio lilisema 26*

*3.1.4 Ufisadi unatengeneza makumi ya mabilionea na kufukarisha mamilioni 28*

*3.2 Maono ya ACT-Wazalendo.............. 34*

*3.2.1 Kuweka Akiba (Savings) na Ukuaji wa Uchumi ........ 40*

*3.2.2 Kupambana na mfumo wa unyonyaji na ufisadi ........ 44*

*3.2.3 Kilimo ........ 47*

*3.2.4 Viwanda ........ 51*

*3.2.5 Utalii ........ 53*

*3.2.6 Madini, Mafuta na Gesi Asilia ........ 55*

*3.2.7 Hitimisho ........ 57*

**SEHEMU YA NNE ........ 61**

*4.1 Miiko ya Uongozi ........ 61*

*4.1.1 Miiko ya viongozi ........ 61*

*4.1.2 Tafsiri ya kiongozi ........ 63*

**NYONGEZA ........ 64**

Hotuba ya kiongozi wa chama Ndugu Zitto Ruyagwa Z. Kabwe aliyoitoa katika uzinduzi wa Chama cha ACT-Wazalendo siku ya Jumapili tarehe 29 Machi 2015 katika ukumbi wa Diamond Jubilee, Dar es Salaam.

# DIBAJI

Mnamo tarehe 26-28 Januari 1967, Halmashauri Kuu ya TANU ilikutana Mjini Arusha. Pamoja na mambo mengine, Mkutano huu ulipitisha Azimio la Arusha. Lengo la Azimio hilo lilikuwa ni kusimika misingi ya ujamaa yenye kuzingatia udugu, umoja, uzalendo, uadilifu na uwajibikaji wa taasisi za umma. Ujamaa huu ulilenga kuujaza umma ujasiri wa kupambana na maadui wakuu watatu, yaani ujinga, maradhi na umaskini.

Mapambano dhidi ya maadui tuliowataja hapo juu yalififishwa na viongozi wa kisiasa kwa kushindwa kuhimili na kukabiliana na wimbi la utandawazi lililokuja na imani ya soko huria lisilozingatia maslahi mapana ya jamii na umma. Aidha, viongozi wa kisiasa na umma kwa ujumla walitumia mwanya wa siasa za utandawazi kujiimarisha katika maslahi binafsi dhidi ya maslahi ya umma na hivyo kuzima ndoto za ujenzi wa siasa na jamii ya kijamaa.

Kwa sababu ya kuzikana siasa za ujamaa na kukumbatia siasa za kibepari, tena ubepari

uchwara unaosambaratisha mfumo wa jamii na kuvunja misingi ya utawala bora na sheria, mfumo wa ufisadi, rushwa na unyonyaji unazidi kujikita nchini mwetu. Kutokana na kutamalaki kwa mfumo wa ufisadi, rushwa na unyonyanji, taifa limejikuta linazalisha matajiri wachache na mamilioni ya watanzania kuendelea kuwa mafukara.

Pamoja na kwamba nchi yetu imejaliwa rasilimali nyingi ambazo, raia wake kwa umoja wao hawafaidiki na rasilimali hizi. Badala yake, uwepo wa rasilimali hizi umechochea migogoro kati ya makundi mbalimbali ya jamii yetu, ikiwemo migogoro kati ya wakulima na wafugaji; migogoro kati ya wanaoitwa wawekezaji na wananchi na hata kati ya serikali na wananchi katika maeneo ya uwekezaji. Mazingira haya yanachangia kuligawa taifa, kulikata vipande vipande na kulinyang'anya umoja na udugu uliojenga misingi ya taifa hili.

ACT – Wazalendo tunaamini kuwa taifa letu linahitaji kurejea katika misingi mama iliyojenga taifa hili, ikiwemo misingi ya umoja, udugu, uzalendo, uadilifu na uwajibikaji wa viongozi na taasisi za umma.

Hivyo basi, Azimio hili la Tabora linalenga kuhuisha misingi mama ya Taifa hili, ikiwemo siasa ya Ujamaa. Hata hivyo, kwa kutambua umuhimu wa demokrasia na haki za binadamu katika mazingira ya dunia ya leo, na kwa kuzingatia mapungufu ya msingi ya kisera katika utekelezaji wa toleo la kwanza la Azimio la Arusha, Azimio hili limezingatia, pamoja na mambo mengine, umuhimu wa demokrasia na mchango wa sekta binafsi katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi hapa nchini.

**Mama Anna Mghwira**
Mwenyekiti wa ACT – Wazalendo Taifa
Juni 2015

ACT
WAZALENDO

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.1 Itikadi, Falsafa, Misingi na Madhumuni ya ACT-Wazalendo

Lengo kuu la siasa ya ujamaa wa kidemokrasia ni kujenga jamii inayozingatia usawa. Ili kujenga jamii yenye kuzingatia na kuishi usawa, chama cha ACT-Wazalendo kitachukua hatua tatu mahsusi zifuatazo:

i) Kuweka mazingira ya kisera yatakayohakikisha kwamba tunapunguza pengo la kipato kati ya mtu na mtu, na kati ya jamii moja na nyingine.

ii) Kuhakikisha kwamba kila mwananchi anakuwa na fursa ya kupata huduma za jamii, ikiwemo elimu na afya

iii) Kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na fursa kikamilifu za kushiriki katika kufanya maamuzi juu ya mambo yanawagusa na kuwakabili binafsi na jamii kwa ujumla.

Aidha, ujenzi wa siasa ya Ujamaa wa kiDemokrasia utazingatia ngao nne zifuatazo:

i) **Udugu** ni hifadhi ya jamii ya asili kwa Waafrika, na hivyo kila mtanzania na kila mwafrika ana jukumu la kumsaidia mwenzake anayekabiliwa na tatizo au janga popote alipo bila kutarajia malipo ya aina yoyote. ACT-Wazalendo itahimiza wananchi kushirikiana kidugu katika kukabiliana na changamoto mbalimbali za kibinadamu, kijamii na kiuchumi na serikali itaweka mazingira ya kufanikisha ushirikiano huo hususani kwamba kila mtu atakuwa na haki sawa ya kupata elimu bora bila malipo yeyote na afya bora kupitia mfumo madhubuti wa Hifadhi ya Jamii;

ii) **Serikali kusimamia maendeleo ya nchi** kwa kuwa na haki na wajibu wa kuendesha moja kwa moja sekta nyeti katika jamii zenye maslahi mapana ya kiusalama na kiuchumi kwa nchi bila kuathiri nafasi ya sekta binafsi

kuendesha shughuli za uzalishaji mali na utoaji wa huduma;

iii) **Viongozi na watumishi wa umma wana** wajibu wa kuhakikisha kwamba wanaishi na kuenenda katika misingi inayolinda heshima ya ofisi za umma na kwamba hawatumii nafasi zao kwa manufaa yao binafsi na jamaa zao. Ili kuwasaidia na kuwawezesha viongozi na watumishi wa umma kuenenda katika misingi ya uadilifu, Miiko ya Viongozi itakuwa ni kanuni ya lazima kufuatwa na kila mtu wenye dhamana ya umma.

iv) **Demokrasia** ndiyo msingi wa maendeleo ya kijamii, kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa na kwamba demokrasia ndiyo msingi wa ujenzi wa taifa huru na linaloheshimu na kuzingatia utawala wa sheria.

Falsafa ya ACT-Wazalendo ni UNYERERE, ikiwa ni dhamira ya kurudisha, kuhuisha na kupigania misingi mama iliyoasisi Taifa la Tanzania, kama ilivyoainishwa katika

ACT WAZALENDO

Azimio la Arusha ambalo lilipitishwa na Halmashauri Kuu ya TANU mwaka 1967 na kama lilivyohuishwa na Chama cha ACT-Wazalendo kwa mazingira ya Tanzania ya sasa, ikiwa na imani kwamba:

i) Binadamu wote ni sawa;

ii) Kila mtu anastahili heshima;

iii) Kila raia ana uhuru kamili wa kutoa mawazo yake, kwenda anakotaka na kuamini dini anayotaka na kukutana na watu wengine bila kuvunja sheria;

iv) Kila mtu ana haki ya kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake na mali yake aliyo nayo kwa mujibu wa sheria;

v) Kila mtu anayo haki ya kupata malipo ya haki kutokana na kazi yake;

vi) Raia wote kwa pamoja wanamiliki utajiri wa asili wa nchi hii ukiwa kama dhamana kwa vizazi vyao na vizazi vijavyo; na

vii) Serikali ina mamlaka na wajibu wa kusimamia njia muhimu za kukuza uchumi.

ACT-Wazalendo itaongozwa na msingi kumi ifuatayo:

### *i) Uzalendo*

Sisi wananchi wa Tanzania tunaipenda nchi yetu. Uzalendo ndio moyo wa kuanzishwa kwa ACT-Wazalendo. Zaidi ya kuipenda nchi yetu, uzalendo ni juu ya kile ambacho tunadhamiria kukifanya na kujitoa katika kuitumikia na kuilinda nchi yetu. Hivyo basi, ubora na umakini wa maamuzi yetu kama chama utapimwa kwa kuangalia ni namna gani maamuzi hayo yana faida kwa taifa letu na wananchi wake kwa leo na kesho.

### *ii) Utu*

Sambamba na Katiba ya nchi yetu na Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu ambalo nchi yetu imeliridhia, utu ni msingi mama kwa chama cha ACT-Wazalendo. Tunatambua thamani ya asili ya ubinadamu na haki za msingi na za asili ambazo binadamu wamepewa tangu uumbaji. Tunaamini kwamba utu ndio msingi wa uhuru, haki, amani na ustawi wa

jamii. Tumedhamiria kupigania, kulinda na kuendeleza maendeleo ya jamii na ustawi wa watu wote na tutapigania na kuheshimu haki za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni kwa watu wote.

### *iii) Kupinga ubaguzi*

Ubaguzi ni adui wa utu na tutaupinga kwa nguvu zote wakati wote na mahala popote. Tunaamini kwamba kila binadamu anastahili heshima na hastahili kubaguliwa kwa sababu ya kabila, rangi, jinsi, lugha, dini, chama cha siasa, utaifa, hali ya kiuchumi, familia anayotoka, afya, ulemavu, n.k. Tunaamini kwamba kila mtu anastahili kupata haki na kwamba maslahi ya makundi yote lazima yazingatiwe katika utungaji wa sera na sheria. Kutokuwa na ubaguzi ni msingi muhimu katika kujenga utaifa na maendeleo shirikishi.

### *iv) Usawa*

Kutokana na miaka mingi ya ubaguzi wa kiuchumi na kijinsia, nchi yetu kwa sasa inapita katika wakati ambao kuna pengo kubwa la kipato katika hali ya kimaisha na

kijamii kati ya maskini, ambao ni kundi kubwa, na matajiri wakiwakilishwa na kundi dogo. Bila kuchukua hatua stahiki wakati huu wa sasa basi maskini watazidi kuwa maskini zaidi. Chama cha ACT-Wazalendo kimeundwa katika msingi wa kuamini kwamba kila mtu ana haki ya kufurahia matunda ya bidii yake katika kazi, na kwamba bidii, umakini na weledi katika kazi ndiyo shina la maendeleo. Tunaamini kwamba tunahitaji kuhuisha misingi ya usawa kwa kuweka mazingira sawa na kuwekeza katika kundi la watu ambao wameachwa nyuma na kunyimwa fursa za kujiendeleza. Tunaamini ni jukumu na wajibu wa serikali kuhakikisha usawa katika jamii kwa kuchukua hatua stahiki za kuwainua wale ambao wapo nje ya mstari na hawafaidiki na ukuaji wa uchumi wa taifa.

### *v) Demokrasia*

Msingi mama wa demokrasia ni kuhakikisha kuwa sauti za watu zinasikika na kuzingatiwa katika mipango ya maendeleo ya nchi. Tunaamini kwamba ni wananchi pekee

wenye uhalali wa kuamua nani awaongoze na aina ya viongozi wanaowataka. Kama chama, kwetu dhana ya demokrasia inakwenda zaidi ya chaguzi za mara kwa mara. Dhana ya demokrasia kwa chama cha ACT-Wazalendo ni sehemu ya mfumo wa uendeshaji wa chama ambapo kila mwanachama anayo nafasi, wajibu na fursa ya kuchangia katika maamuzi ya chama na nchi, na anayo haki ya kuomba kuchaguliwa katika ngazi yoyote ya uchaguzi.

### *vi) Uhuru wa Mawazo na Matendo*

Jamii yoyote ya kidemokrasia inategemea uwepo wa uhuru wa kutofautiana kimawazo na fursa ya kila mtu kutoa maoni yake bila woga. Tunaamini kwamba watu wanapaswa kuwa na uhuru wa matendo ili mradi tu matendo yao hayaingilii haki za watu wengine wala kuvunja sheria. Tunaamini kwamba ubunifu ni zao la mchango wa mawazo tofauti kutoka kwa watu tofauti. Hivyo, chama kitalea na kuhamasisha utamaduni wa uhuru wa mawazo kama njia ya kuendelea kujifunza njia bora zaidi za kuboresha maisha ya watanzania.

### *vii) Uadilifu*

Tunaamini kwamba kura ni tendo la imani linaloonyeshwa na mwananchi kwa viongozi anaowachagua. Uaminifu wa wananchi unapaswa kuheshimiwa kwa kuonyesha uadilifu wa hali ya juu kutoka kwa viongozi. Sisi kama chama tutasimamia uadilifu kwa umakini mkubwa kama njia muhimu ya kujenga imani na kuwapa heshima wale wanaotuamini katika kuwatumikia. Ili kuhakikisha kwamba tunatekeleza msingi huu kikamilifu, tumetengeneza kanuni za mwenendo wa maadili na miiko ya uongozi ambayo kila kiongozi wa chama cha ACT-Wazalendo na serikali itokanayo atasaini kukubali kuwa tayari kuwajibika na kuwajibishwa kwayo. Maadili na miiko ya uongozi itakuwa ndiyo dira ya mwenendo wa viongozi wote wa chama cha ACT-Wazalendo katika utumishi wa umma na ambao tungependa umma wa watanzania utuwajibishe nao.

### *viii) Uwazi*

Ili wananchi waweze kuwawajibisha viongozi wao ni lazima wawe na taarifa sahihi na kwa wakati unaofaa. Tunaamini kwamba wananchi wana haki ya kupata taarifa sahihi na kwa wakati kutoka kwa viongozi wao na ofisi zote za umma kwa kuwa viongozi wanafanya kazi na kusimamia raslimali za chama na taifa kwa niaba ya wananchi. Katika kutekeleza msingi huu, viongozi wote wa ACT watapaswa kueleza wanachama na wananchi kuhusu mali wanazomiliki katika maeneo yao ya uongozi, kabla na baada ya kuchaguliwa au kuteuliwa. Aidha, programu zote za chama pamoja na mapato na matumizi zitawekwa wazi kwa umma na wanachama na wananchi wataruhusiwa kuzikagua wakati wowote.

### *ix) Uwajibikaji*

Bila kujenga utamaduni wa kuwajibishana hatutaweza kama taifa kujenga jamii ambayo kila mtu anaheshimiwa na kuheshimu sheria ambazo tumejiwekea. Uwajibikaji unapaswa kuanza na viongozi waliopewa dhamana ya kuongoza harakati

za mabadiliko katika nchi. Katika chama cha ACT-Wazalendo, tunaamini kwamba kila mtu anayetupigia kura ametuamini na kuweka matumaini yake kwetu kwamba tunaweza kutekeleza kile tunachosema. Tunaamini pia kwamba wanachama na viongozi wanapaswa kuwajibishwa kwa matendo na ahadi wanazozitoa kwa wananchi.

### *x) Umoja*

Umoja ndiyo nyenzo muhimu ya kukabiliana na changamoto ambazo zinatukabili leo na kesho. Kama nchi ambayo imejaliwa utajiri na tofauti za kijamii mbalimbali kama vile utamaduni, makabila, dini, lugha, na siasa, tunahitaji kusimama pamoja ili kuweza kujenga taifa moja la Tanzania ambalo kila mmoja anafurahia kuwa sehemu yake. Kwa hiyo mapambano na shida za kundi moja ni mapambano na shida zetu sote. Kwa kuzingatia historia yetu ya kupigania umoja na maelewano katika bara la Afrika na duniani kwa ujumla, chama cha ACT-Wazalendo kinatambua umuhimu wa umoja na ushirikiano na majirani zetu na

hivyo itashirikiana na nchi nyingine katika kusukuma mbele ajenda ya Umoja wa Afrika ili kuweza kujenga nguvu za pamoja katika kujiendeleza kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa.

# SEHEMU YA PILI

## 2.1 Siasa ya Ujamaa wa kidemokrasia na ndoto ya Tanzania

Tanzania ni zaidi ya mkusanyiko wa watu na vitu vilivyomo. Msingi wa ujenzi wa Taifa ni UZALENDO unaochochewa na itikadi, falsafa na imani imara. Hata hivyo, katika siku za karibuni utaifa wa Taifa la Tanzania umetikiswa. Nchi sasa imeanza kugeuka kuwa mkusanyiko tu wa watu wanaohangaika kutafuta vitu na ambao wanatumia muda mwingi kuimarisha 'vitaifa' vyao kupitia vyama vyao vya siasa, dini zao na hata makabila yao. Hii inatokana na kukosekana kwa itikadi moja ya kitaifa yenye kuweza kuunganisha makabila zaidi ya 124 yaliyopo nchini na wafuasi wa dini zote.

Hivyo basi, chama cha ACT-Wazalendo kinalenga kuhuisha misingi iliyoimarisha taifa na sera zake zitalenga kufufua uzalendo, upendo, umoja na mshikamano

wa watanzania wote bila kujali rangi, kabila, dini, jinsia na wala ufuasi wa chama cha siasa. Chama cha ACT-Wazalendo kinalenga kufufua utaifa wa Tanzania ili kila Mtanzania aone kuwa ana wajibu wa kujenga nchi yake ili kutimiza ndoto ya kuwa na **Taifa lenye kujitegemea kiuchumi na kiutamaduni, na ambalo linalinda na kudumisha usawa, ustawi wa jamii, uwajibikaji, demokrasia, na uongozi bora.**

Ili ndoto hii itimie, ni sharti kuzingatia kwamba:

### *i) Hakuna unyonyaji*

Nchi yenye Ujamaa wa kidemokrasia haina unyonyaji maana kila mtu huwajibika kufanya kazi na kupata malipo anayostahili kulingana na kazi yake. Katika Nchi ya aina ya ujamaa tunaotaka kujenga, Serikali kwa kupitia sera za kodi na sera za nchi hurekebisha tofauti ya kipato kati ya walionacho na wasio nacho. Nchi yetu hivi sasa imekuwa na matabaka makubwa kiasi kwamba wakulima, wafanyakazi, wavuvi, wafugaji na wafanyabiashara ndogo

ndogo wananyonywa na watu wenye mitaji mikubwa na wawekezaji wa nje. Ili kujenga mfumo wa ujamaa wa kidemokrasia ni lazima kuondoa vikundi maslahi vya kinyonyaji (cartels) katika uchumi na wajibu huu ni wajibu wa Dola. Vile vile ni lazima kuwezesha wananchi kufanya shughuli za uzalishaji mali kwa uhuru na bila bugudha kwa kuweka sera zinazozuia watu wa kati (middlemen) na kuhakikisha upatikanaji wa mitaji kwa wananchi wa kawaida.

### *ii) Uchumi imara, shirikishi na unaosimamiwa na dola*

Watawala walipoamua kulizika Tamko la Arusha na Azimio la Arusha walielekeza taifa katika sera za kiliberali na kibwanyeye ambapo uchumi uliendeshwa na soko holela. Hii ilirejesha umiliki wa uchumi kwa watu wachache wenye mitaji. Viwanda, Mabenki, Njia za Usafirishaji, Bima, Biashara ya ndani na ya kigeni vyote vilimilikishwa kwa watu binafsi. Madhara yake ni kwamba watu wachache na hasa wageni wameshika uchumi wa nchi na wanafanya watakalo.

Wakati mwishoni mwa miaka ya sabini, Tanzania ilikuwa na uwezo wa kubangua korosho zote zinazozalishwa nchini, hivi sasa korosho yote inauzwa nje ikiwa ghafi na kukosesha Taifa mapato mengi ya fedha za kigeni. Mabenki yameshikwa na wageni na hivyo Taifa kushindwa kusimamia sera zake za fedha za kigeni ipasavyo.

Namna pekee ya kujenga na kudumisha ujamaa wa kidemokrasia ni kubomoa 'cartels' na kuwezesha wananchi wengi zaidi kumiliki uchumi kupitia Serikali yao au vyama vyao vya ushirika na jumuiya za wananchi. Dola inapaswa kusimamia uchumi ipasavyo kwa kutunga sera za makusudi zenye kuwezesha uzalishaji mkubwa wa ndani. Vile vile iwe ni marufuku kwa watu binafsi kumiliki miundombinu kama barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, mifereji ya umwagiliaji, nguvu za umeme, mkonga wa Taifa na viwanda mama kama vile chuma na makaa ya mawe na visima vya mafuta na gesi. Watu na makampuni binafsi wanaweza kuhusika kwenye uendeshaji (operatorship) kwa makubaliano maalumu na Serikali.

# SEHEMU YA TATU

## 3.1 Hali ya nchi na Matamko ya kisera

### *3.1.1 Kumomonyoka kwa umoja na kukithiri kwa rushwa na umaskini*

Ni dhahiri kwamba nchi yetu hivi sasa ina nyufa na hasa nyufa katika umoja wetu na kuporomoka kwa maadili. Udugu na utu unazidi kumomonyolewa. Leo hii, kwa mfano, ikitokea mtu amepata ajali barabarani, badala ya watu kumsaidia, watu wengi humuongezea maumivu kwa kumpora na kumnyang'anya vitu alivyokuwa navyo. Huko nyuma jamii nzima iliweza kuwajibika kumlea mtoto yeyote popote alipo, lakini leo Tanzania inazalisha watoto wa mitaani kila siku kwa kuwa tu hawana wazazi wa kubailojia au wazazi waliopo hawana uwezo wa kiuchumi wa kuwatunza. Undugu na udugu umefifia na uko hatarini kutoweka.

Hatuamini tena kwamba mafanikio hutokana na kujitegemea na bidii katika kazi. Tumegeuka kuwa taifa la ombaomba na kuishi kwa ujanjaujanja. Wezi wa mali za umma wanasifiwa na kuchekewa. Uongozi na utumishi wa umma umekuwa ndiyo njia ya kujipatia utajiri badala ya kutumikia wananchi. Uongozi na utumishi wa umma umegeuka kuwa tiketi ya kujitajirisha kupitia kujilipa posho kubwa na mishahara mikubwa na stahili kadha wa kadha bila kujali hali ya nchi yetu kiuchumi. ACT-Wazalendo tunasema hali hii **haikubaliki na lazima turudi katika misingi!**

Tanzania hivi sasa ni moja ya nchi masikini zaidi duniani licha ya utajiri mkubwa wa watu, maliasili na eneo la kijiografia. Takwimu za maendeleo ya binadamu zinaonyesha kuwa Tanzania ni nchi ya 159 kwa umasikini kati ya nchi 187 duniani. ACT-Wazalendo tunasema hali hii **haikubaliki!**

Baadhi ya wanazuoni wamewagawa Watanzania katika madaraja matatu: Walalahoi, Walalaheri na Walalahai

wakimaanisha watu wenye kuishi kwenye dimbwi la umasikini, watu wenye ahueni na matajiri. Pia kuna daraja jipya la 'wakeshahoi'. Hawa wa mwisho ndio hao wanaitwa 'masikini wa kutupwa' kwa lugha ya mtaani. Watanzania ni masikini kwa sababu watawala wetu wameamua hivyo kwa kutunga na kutekeleza sera na mikakati ambayo inanufaisha watu wachache katika tabaka la juu la maisha ambao wengi wanaishi mijini na kuacha watu wengi wanaoishi vijijini wakiwa masikini zaidi. ACT-Wazalendo tunasema hali hii **haikubaliki na lazima turudi katika msingi wa kukifanya kila kijiji kuwa kitovu cha maendeleo ya taifa!**

### *3.1.2 Mfumo wa uchumi unaonyonya wananchi vijijini*

Mfumo wa uchumi wa nchi yetu bado ni wa kinyonyaji. Kwamba wakazi wa mijini wanafaidi zaidi rasilimali za nchi kuliko wakazi wa vijijini. Mfumo wa uchumi wa Tanzania ni wa kifisadi na ufisadi unafaidisha kikundi kidogo cha watu mijini au wenye tabia za kimjini na hivyo kukosesha huduma za msingi za wananchi

wengi waishio vijijini. Tazama mifano hii hapa chini:

- Kuongezeka kwa kasi kwa tofauti ya kipato kati ya walionacho na wasionacho ambapo sasa kuna kundi dogo la watu matajiri sana na kundi kubwa sana ni la watu fukara sana. Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 30 ya Watanzania wanamiliki asilimia 75 ya Pato la Taifa. Kwa kutumia vigezo mbalimbali vya kupima kiwango cha Umasikini (MPI 2013), asilimia 64 ya Watanzania ni masikini na asilimia 31.3 wanaishi katika umasikini uliokithiri. Kwa hiyo ni asilimia takribani tano (5%) ya watanzania ndiyo wenye maisha ahueni au matajiri.

- Kasi ya kupunguza umasikini nchini inaonekana mijini kuliko vijijini ambapo katika kipindi cha miaka 16, umasikini wa watu wa Dar es Salaam, kwa mfano, umepungua kwa asilimia 12 wakati umasikini vijijini umepungua kwa asilimia 2 tu. Ripoti

ya Maendeleo ya Binadamu ya Taifa ya Mwaka 2014 kuhusu Tanzania inaonyesha kuwa Watanzania masikini zaidi wanaishi mikoa ya Kigoma, Singida, Dodoma, Kagera, Tabora, Shinyanga na Pwani.

- Kasi ya ukuaji wa uchumi wa vijijini ipo chini ya wastani wa ukuaji wa uchumi wa Taifa kutokana na sekta ya kilimo, ambayo inaajiri asilimia 75 ya Watanzania, kuwa na ukuaji mdogo mno wa asilimia 4 wakati uchumi wa nchi umekuwa ukikua kwa wastani wa asilimia 7 katika muongo mmoja uliopita. Asilimia 67 ya kaya nchini kwetu zinaishi katika makazi yenye sakafu za udongo, mchanga au kinyesi cha ng'ombe. Asilimia 63 ya kaya za Tanzania hazipati maji ya bomba.

Hali hii inasababishwa na ukweli kwamba fursa nyingi za kiuchumi na maendeleo kwa ujumla zimekuwa zikitolewa kwa watu wa mijini zaidi kuliko vijijini na kwamba mfumo wetu wa maendeleo ya uchumi na kijamii umewanyima fursa watu waliopo

ACT WAZALENDO

vijijini. Hali hii ilijitokeza pia wakati Azimio la Arusha linapitishwa mwaka 1967 pale ambapo Mwalimu Nyerere alisema, tunanukuu:

*"Vile vile mkazo wa fedha na wa viwanda unatufanya tukazanie zaidi maendeleo ya mijini. Tunatambua kuwa hatuwezi kupata fedha za kutosha kuleta maendeleo katika kila kijiji na ambayo yatamfaa kila mwananchi. Tunajua pia kuwa hatuwezi kujenga kiwanda katika kila kijiji ili kisaidie kuleta maendeleo ya fedha na viwanda katika kila kijiji; jambo ambalo tunajua kuwa haliwezekani. Kwa ajili hiyo, basi, fedha zetu huzitumia zaidi katika miji na viwanda vyetu pia hujengwa katika miji. Na zaidi ya fedha hizi huwa ni mikopo na hatimaye lazima zilipwe.*

*Lakini ni dhahiri kwamba haziwezi kulipwa kwa fedha zinazotokana na maendeleo ya mijini au maendeleo ya viwanda. Hazina budi zilipwe kwa fedha tunazopata kutokana na vitu tunavyouza katika nchi za nje. Kutokana na viwanda vyetu hatuuzi na kwa muda mrefu sana hatutauza vitu vingi katika nchi za nje. Viwanda vyetu zaidi ni vya*

ACT WAZALENDO

*kutusaidia kupata vitu hapa hapa ambavyo mpaka sasa tunaviagiza kutoka nchi za nje. Itapita miaka mingi kabla ya kuweza kuuza katika nchi za nje vitu vinavyotokana na viwanda vyetu. Kwa hiyo ni dhahiri kwamba fedha tutakazotumia kulipa madeni haya ya mikopo ya fedha kwa maendeleo na viwanda mijini hazitatoka mijini na wala hazitatokana na viwanda. Zitatoka wapi, basi? Zitatoka vijijini na zitatokana na KILIMO. Maana ya ukweli huu ni nini? Ni kwamba wale wanaofaidi maendeleo yanayotokana na fedha tunazokopa sio kwa kweli watakaozilipa. Fedha zitatumika zaidi katika miji lakini walipaji watakuwa zaidi ni wakulima.*

*Jambo hili linafaa kukumbukwa sana, maana kuna njia nyingi za kunyonyana. Tusisahau hata kidogo kwamba wakaaji wa mijini wanaweza wakawa wanyonyaji wa jasho la wakulima wa vijijini. Hospitali zetu kubwa zote ziko katika miji. Zinafaidia sehemu ndogo sana ya wananchi wa Tanzania. Lakini kama tumezijenga kwa fedha za mkopo walipaji wa mkopo huo ni wakulima, yaani wale ambao hawafaidiwi sana na hospitali*

*hizo. Mabarabara ya lami yako katika miji, kwa faida ya wakaaji wa mijini na hasa wenye magari. Kama mabarabaraba hayo tumeyajenga kwa fedha za mikopo walipaji ni wakulima; na fedha zilizonunua magari yenyewe zilitokana na mazao ya wakulima. Taa za umeme, maji ya mabomba, mahoteli na maendeleo mengine yote ya kisasa yako zaidi katika miji. Karibu yote yametokana na fedha za mikopo na karibu yote hayana faida kubwa kwa mkulima, lakini yatalipwa kwa fedha zitakazotokana na jasho la mkulima.*

*Tusisahau jambo hili. Japo tunapotaja unyonyaji hufikiria mabepari, tusisahau kuwa bahari ina samaki wengi. Nao hutafunana. Mkubwa humtafuna mdogo na mdogo naye humtafuna mdogo zaidi. Katika nchi yetu twaweza kugawa wananchi kwa njia mbili. Mabepari na Makabaila upande mmoja; na wafanyakazi na wakulima upande mwingine. Pia twaweza tukagawa wakaaji wa mijini upande mmoja na wakulima wa vijijini upande mwingine. Tusipoangalia tutakuja kugundua kuwa wakaaji wa mijini nao ni wanyonyaji wa wakulima."* Azimio la Arusha,1967. (msisitizo ni wetu).

Azimio la Arusha limerudia zaidi ya mara moja “Tusisahau jambo hili” ama “Jambo hili linapaswa kukumbukwa sana”. Ni dhahiri kuwa tumesahau jambo hili na hivyo maendeleo vijijini kuwa ni hadithi tu za wanasiasa.

Licha ya kwamba wanasiasa wa kisasa wanaona Azimio la Arusha ni nyaraka iliyopitwa na wakati, sisi ACT-Wazalendo tunaamini kwamba maana ya kurudi katika misingi ni kurudi katika misingi ya Azimio la Arusha. Mwangwi wa “tusisahau jambo hili” lazima uendelee kutuonyesha kuwa kuna kazi ya kufanya kuhusu mafukara mamilioni wanaoishi kwenye vijiji vyetu. Watanzania hawa wa vijijini hawana fursa za barabara, maji, umeme na hata huduma za jamii kama wenzao wa mijini. Kwa mfano, Taarifa ya Taifa ya Maendeleo ya Binadamu ya Mwaka 2014 inaonyesha kwamba ni asilimia 8 tu ya kaya za vijijini zenye umeme kwa ajili ya mwanga, wakati mijini ni asilimia 49. ACT –Wazalendo tunasema hili **halikubaliki** na **lazima turudi katika misingi!**

Ukiangalia Bajeti ya nchi yetu Tanzania hivi sasa utaona namna ambavyo rasilimali kubwa ya nchi inatumika kutatua changamoto za watu wa mijini na hasa Dar es Salaam. Wabunge (ambao wengi wanatumia muda mwingi sana Dar es Salaam) bila kujali majimbo au mikoa yao hukasirikia sana, kwa mfano, foleni Dar es Salaam na kuisukuma Serikali kutenga fedha zaidi za kujenga barabara za Dar es Salaam. Umeme ukikatika Dar es Salaam, waandishi wa habari wanaandika 'nchi gizani' bila kujali kuwa Watanzania wa Urughu kule Iramba na wengine asilimia 92 ya Watanzania wapo kwenye giza la kudumu. Zaidi ya fursa walizonazo, masikini wa mijini pia sauti zao zinasikika. Mafukara wa vijijini nadra kuwasikia na huishia tu kukugumia shida zao.

### *3.1.3 Tusisahau jambo hili, Azimio lilisema*

Masikini wanaoishi vijijini licha ya kufanya kazi kwa bidii na hasa kazi za kilimo hawana fursa za kuondokana na umasikini. Mfumo wa uchumi wa nchi umejengwa kwa misingi kwamba watu wa vijijini

hupokea bei za kuuza mazao yao kutoka mijini na vilevile hupokea bei za kununua bidhaa zinazotengenezwa mijini kutoka huko huko. Mkulima wa Peramiho huuza mahindi yake kwa bei ya kijijini iliyo chini (tena kwa mkopo) na anapotaka kununua sukari hulipa bei kubwa kuliko hata bei ya Songea Mjini.

Barabara za vijijini zina hali mbaya au hazipo kabisa. Huduma za jamii kama elimu, maji na afya ni mbaya. Huduma za nishati ya umeme hazipo kabisa katika nyumba 92 kati ya 100 za vijijini hapa nchini. Masikini wa vijijini ni mafukara. Wamefukarishwa kutokana na sera zinazonyonya jasho la kazi yao kwa upande mmoja na sera zinazowanyima maendeleo ya miundombinu kwa upande mwingine.

Kufunguliwa kwa miundombinu ya vijijini kama barabara, maji na nishati ya umeme kunaweza kuwaondoa watu wa vijijini kwenye minyororo ya ufukara. Huduma bora za elimu, afya na uhakika wa masoko ya mazao na hifadhi ya jamii vinaweza hatimaye kutokomeza kabisa umaskini.

ACT WAZALENDO

Lakini, watawala wanaogawa rasilimali ya nchi hawataki. Wanasema hakuna rasilimali fedha za kutosha kusambaza umeme vijijini ili kukuza viwanda vidogo vidogo na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, kusambaza maji safi na salama ili kuboresha afya na kumpunguzia mwanamke wa kijijini muda wa kutafuta maji na kujenga barabara za vijijini ili wakulima wafikishe mazao yao sokoni. Ikifika kujenga shule na zahanati na vituo vya afya, wananchi wa vijijini wanaambiwa wajenge wenyewe, wajitolee. ACT-Wazalendo tunasema hali hii **haikubaliki na lazima turudi katika misingi!**

### *3.1.4 Ufisadi unatengeneza makumi ya mabilionea na kufukarisha mamilioni*

Kwa vipindi tofauti katika miaka ya karibuni, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limekuwa likiibua kashfa mbalimbali zinazoonesha namna ambavyo fedha za nchi zinavyoibwa na wachache. Tumeshuhudia, kwa mfano:

- Ufisadi uliofanywa Benki Kuu ya Tanzania kwa kuibwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 133 za Akaunti ya Malipo ya Nje (EPA),

- Utoroshaji mkubwa wa fedha zilizofikia dola za Kimarekani milioni 136 kupitia mradi wa Meremeta uliokuwa chini ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (TPDF),

- Uingiaji wa mkataba wa madini ya dhahabu wa Buzwagi uliokuwa na thamani ya dola za Kimarekani milioni 400 bila kuzingatia uhitaji wa kuboresha mazingira ya nchi kufaidika na utajiri wa madini; na

- Wizi mkubwa wa fedha za msaada wa kuagiza bidhaa kutoka Serikali ya Japan (Commodity Import Support) ambapo zaidi za shilingi bilioni 40 ziligawiwa kwa viongozi kadhaa wa serikali na wafanyabiashara.

- Kashfa kubwa ya Mkataba wa Umeme wa Richmond ambayo ilipelekea nchi

ACT WAZALENDO

kukaa gizani kwa muda mrefu na kuzorotesha shughuli za uzalishaji mali na kuathiri uchumi.

- Kashfa kubwa sana ya Tegeta Escrow Account ambapo zaidi ya shilingi bilioni 306 zilichotwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

- Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kuonyesha namna ubadhirifu ulivyokithiri katika matumizi ya fedha za Umma. Takribani asilimia 30 ya bajeti kwenye manunuzi ya umma huishia kwenye mikono ya watu wachache.

ACT WAZALENDO

- Kashfa kubwa ya Watanzania wanaoficha fedha katika benki za nje ya nchi ambapo Benki Kuu ya Shirikisho la Uswisi ilitangaza kwamba Watanzania wamehifadhi zaidi ya shilingi bilioni 334 katika fedha za kigeni kwenye mabenki ya nchi hiyo.

Katika Kitabu cha 'Africa's Odious debts: How foreign loans and capital flight bled a continent', waandishi Leonce Ndikumana na James Boyce, wameonyesha kwamba katika kipindi cha miaka 40 jumla ya dola za Kimarekani 11.4 bilioni zimetoroshwa kutoka Tanzania kwa njia mbalimbali. Hizi ni sawa na wastani wa dola za Kimarekani 285 milioni kutoroshwa kila mwaka kuanzia mwaka 1970 mpaka 2010. Sehemu kubwa ya fedha hizi zinatoroshwa na makampuni makubwa ya kigeni yanayofanya biashara na kuwekeza hapa nchini (utoroshaji mkubwa umefanyika mara baada ya Tanzania kuanza kuzalisha dhahabu kwa wingi na makampuni makubwa ya nje kuanza kutafuta mafuta na gesi asilia kwenye bahari ya Tanzania) na sehemu nyingine ni bakshishi wanayopewa viongozi na maafisa wa serikali wanaofanikisha utoroshaji huu.

Utafiti uliofanywa na Africa Progress Panel na kikosi kazi kilichoongozwa na aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini Bwana Thabo Mbeki unaonyesha kuwa Afrika hupoteza zaidi ya dola za kimarekani 50 bilioni kila mwaka kutokana na utoroshaji unaofanywa na makundi haya. Huu ni mtaji mkubwa unaotumika na mataifa ya magharibi

kuendeleza nchi zao na kuendelea kuzinyonya nchi za Kiafrika. Makampuni makubwa ya kimataifa kwa kushirikiana na wananchi hutorosha fedha hizi na kulikosesha bara la Afrika na Tanzania chanzo kikubwa cha mitaji katika soko la mitaji.

Watanzania hawa (wanasiasa, watendaji, maafisa wa Jeshi na Usalama wa Taifa na wafanyabiashara) huficha fedha hizi chafu kwenye mabenki ughaibuni na hasa Uswisi, Dubai, Mauritius, Afrika Kusini na maeneo mengine (Tax Havens/ Offshore/Treasure Islands). Wengine wamewekeza kwenye mali zisizohamishika kama majumba na zinazohamishika kama hisa kwenye makampuni mbalimbali duniani.

Rushwa na ufisadi vinatengeneza Watanzania wachache kuwa mabilionea. Mabilionea hawa ambao wana ushawishi mkubwa katika kuunda sera za nchi na utekelezaji wake wanasababisha kuundwa kwa sera na sheria zinazolinda utajiri wa walionacho na kuendelea kuhakikisha maskini wanaendelea kuwa mafukara.

Rasilimali za nchi zinaboresha maeneo ambayo mabilionea na wasaidizi wao wanaishi na kusahau kabisa kwamba Watanzania wengi wanaishi vijijini

na huko ndiko kuna umaskini mkubwa. Umaskini wa vijijini kwa kiasi kikubwa unatokana na sera na matendo yanayofukarisha wananchi wengi. Ukuaji wa uchumi unaoambatana na ufisadi wa kiwango kinachotokea Tanzania unawafanya wenye nacho kupata zaidi na masikini kuwa mafukara zaidi. ACT-Wazalendo tunasema hili **halikubaliki na lazima turudi katika misingi!**

Tunaweza kujenga taifa la watu sawa kwa kufanya maamuzi ya kubomoa mfumo wa kiuchumi wa kinyonyaji ambao umejengwa tangu kupata uhuru. Juhudi za kujenga taifa lenye watu sawa ziliyeyuka mara baada ya kuamua kutelekeza Azimio la Arusha na kufuata sera za ubinafsishaji ambapo zilitafsiriwa kwa kukabidhi mali za taifa kwa kundi dogo la watu na hivyo kutengeneza mfumo wa kifisadi ambao sasa umeota mizizi. Kazi iliyofanywa kwa miaka ishirini ya kujenga uchumi wa viwanda ziliyeyushwa katika kipindi cha miaka mitano tu ambapo viwanda vyote viligawanywa kwa watu binafsi na vingi leo ni maghala tu ya kuhifadhia bidhaa nyingine.

Kutochukua maamuzi madhubuti ya kutokomeza ufisadi na mfumo wake ni kufukarisha Watanzania kwa sababu rasilimali ambayo inapotea kupitia

vitendo vya kifisadi ingeweza kuwekezwa katika maendeleo ya watu wa vijijini, kwa kukuza shughuli za kiuchumi na kupanua mapato ya wananchi.

## 3.2 Maono ya ACT-Wazalendo

Jambo moja la msingi la kuzingatia tunapohuisha Azimio la Arusha ni kwamba mazingira yamebadilika. Mwalimu Nyerere na wenzake walifanya tathmini ya hali ya kipindi ambacho Taifa lilitegemea sana mazao ya kilimo kwenye mauzo ya nje. Ndio maana mara kadhaa Mwalimu Nyerere alipata kusema 'tunanunua trekta moja kwa tani 15 za chai' akilinganisha urari wa biashara kati ya tunachouza nje na tunachonunua kutoka nje. Hivi sasa hali imebadilika na hivyo Azimio lililohuishwa ni vema lizingatie muundo wa sasa wa kiuchumi na kuufanyia mageuzi makubwa (transformation) ili kujenga uchumi shirikishi (inclusive economy).

Ni muhimu kuwa tayari kubadilika kulingana na mabadiliko katika dunia na nchini kwetu. **Ujamaa wa kiDemokrasia**

**wenye kuelekea kujenga dola la kimaendeleo (developmental state) na wenye kuzingatia mila na utamaduni wa kitanzania ndio njia tunayopaswa kwenda hivi sasa.** Swali muhimu la kujiuliza wakati wote ni kama njia tunayochukua itajibu changamoto zetu za Maendeleo? Tukisha chagua njia tunayotaka ni lazima tuwe na imani thabiti kwa njia hiyo na kuhakikisha kuwa maamuzi yetu yanatokana na ukweli na ukweli huo lazima ujaribiwe kwa vitendo. Hatuna budi kubomoa mfumo uliopo sasa na kujenga mfumo madhubuti utakaokuwa njia ya msingi tuliyochagua kwa ajili ya kujenga Dola la Kimaendeleo ili kutimiza ndoto yetu.

ACT WAZALENDO

Mazingira ya sasa yanataka sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kuendesha uchumi na Serikali kusimamia na kudhibiti njia kuu za uchumi na kuendesha huduma za msingi kama Elimu na Afya, Maji, Umeme na miundombinu.

Azimio la Arusha lilitafsiri kuwa ujasiriamali (entrepreneurship) ni unyonyaji; Kwamba mtu mwenye kiwanda akifanyiwa kazi na

watu aliowaajiri ni mnyonyaji; Kwamba mtu mwenye shamba akilimiwa na vibarua aliowaajiri ni mnyonyaji. Kwa ACT – Wazalendo, unyonyaji ni kutompa mtu ujira stahiki kulingana na kazi yake. Uchumi ni lazima uwe na watu wanaofikiria na kubuni shughuli za uzalishaji na walipwe kulingana na ujasiriamali wao bila ya kunyonywa kwa kazi zao. Kama ambavyo nguvu kazi (labour force) hulipwa kwa mshahara, mtaji hulipwa kwa riba na ardhi hulipwa kwa tozo (rent), ndivyo ujasiriamali hulipwa kwa faida. Ni wajibu wa Dola kudhibiti ulimbikaji wa mali kupitia mfumo wa kodi kama ilivyo kwa nchi za Skandinavia sio kuzuia wajasiriamali kubuni biashara na kupata faida (reward) kulingana na ubunifu na usimamizi wa biashara zao.

**Mazingira ya sasa ya nchi kama Tanzania yanataka ongezeko la uzalishaji mali na tija katika uzalishaji ili kuongeza uwezo wa Taifa kuhudumia wananchi wake. Mazingira ya sasa yanahitaji kujenga uwezo mkubwa wa kujiwekea akiba ili kuhimiza ukuzaji wa mitaji ya ndani ili kuongeza uwezo wa kuzalisha mali,**

**ubunifu na maendeleo ya teknolojia. Mazingira ya sasa sio ya kutaifisha na kubinafsisha kila kitu, bali ni ya kumilikisha wananchi uchumi wao na kuuondoa kwenye mikono ya wachache.** Tanzania ya sasa inataka soko la mitaji kumilikiwa na wananchi wengi kwa msaada wa dola. Ni vema kuzingatia jambo hili kila wakati tunapohuisha Azimio la Arusha.

Jambo jingine ni kwamba Azimio lililohuishwa lazima lizingatie uzalishaji mali badala ya kujikita kwenye mgawanyo wa kidogo kilichozalishwa. Mwaka 1977 Mwalimu Nyerere alisema "Kwa miaka kumi tumefanya vizuri sana katika kusambaza huduma za msingi za kijamii kwa watu wengi vijijini. Bado kuna kazi zaidi ya kufanya; lakini tunaweza kufanya hivyo iwapo tu tutazalisha zaidi mali. Hatujaweza kufanya hivyo".

Mwaka 1967 sekta ya Kilimo (ikiwemo uwindaji, ufugaji na misitu) ilikuwa inachangia 80% ya Pato la Taifa (GDP), viwanda na huduma vilichangia kiwango kilichobakia. Kipindi hicho zao moja tu

la Mkonge lilikuwa linaingiza takribani theluthi mbili ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya nje ya nchi.

Mwaka 2014 sekta za kilimo na viwanda vimechangia 50% ya Pato la Taifa (Kilimo 26%, Viwanda 24%), wakati sekta ya huduma inachangia nusu iliyobakia. Mapato ya fedha za kigeni yanachangiwa na utalii kwa zaidi ya dola za kimarekani bilioni mbili, viwanda dola bilioni moja na nusu na dhahabu dola bilioni moja na milioni mia mbili. Biashara ya bandari (transit trade) inaingiza fedha nyingi zaidi za kigeni kuliko mazao yote ya kilimo ambayo yanaingiza dola milioni mia saba tu.

ACT WAZALENDO

Changamoto kubwa ya Tanzania ni kutokubadilika kimaendeleo kwa sekta ya kilimo wakati bado inaajiri watu wengi sana nchini. Hiki ndicho kiini cha umasikini wa Tanzania. Azimio la Arusha linalohuishwa lazima lijibu changamoto hii kwa kuelekeza uundwaji wa sera zitakazoongeza uzalishaji nchini kwenye sekta zote na maradufu kwenye sekta ya kilimo na viwanda vya

bidhaa za kilimo. Hili litawezekana iwapo taifa litawekeza vya kutosha kwenye kilimo na ili kupata fedha za kuwekeza hatuna budi kuongeza uwekaji akiba nchini.

Hifadhi ya Jamii kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wote walio katika sekta isiyo rasmi ni moja ya njia ya kuongeza uwekaji akiba nchini na kuwalinda watu kwenye makundi hayo dhidi ya majanga ya kiuchumi na kijamii. Shirika la Kazi la Dunia (ILO) linathibitisha kwamba "Nchi zilizofanikiwa sana kwenye kuongeza tija kukiwa na mifumo ya hifadhi ya jamii ziliongeza kasi ya ukuaji uchumi kwa nukta moja zaidi kuliko nchi nyingine zinazoendelea". Uwekaji akiba nchini hivi sasa ni mdogo kwa kiwango cha 16% tu ya Pato la Taifa wakati nchi kama Uchina wananchi wao huweka akiba mpaka 50% ya Pato la Taifa. Ili kuhimiza uwekaji akiba nchini inabidi kuweka vivutio kwa Serikali kuchangia theluthi ya kiwango cha chini cha mchango ambao mwananchi (Mkulima, Mfugaji, Mvuvi, Mfanyabiashara ndogondogo na yeyote asiye kwenye sekta rasmi) anachangia kwenye mfumo wa Hifadhi ya

Jamii, kuweka fao la Bima ya Afya kwa kila mchangiaji na fao la Bei kwa Mazao (Price Stabilization Benefit) kwa wakulima.

Ili Taifa letu liweze kujitegemea kiuchumi, hatua zifuatazo zitachukuliwa:

### *3.2.1 Kuweka Akiba ( Savings ) na Ukuaji wa Uchumi*

Kwa miaka takribani kumi na mitano (2000 – 2015) Tanzania imekuwa na uchumi unaokua kwa kasi ya wastani wa 7% kwa mwaka. Hata hivyo kasi hii ya kukua kwa uchumi imeshindwa kuondoa umasikini wa wananchi kwani kwa kiasi kikubwa kasi hii imesukumwa na mitaji kutoka nje ambayo imewekezwa kwenye sekta ambazo haziwanufaishi wananchi moja kwa moja kama vile Madini, Mafuta na Gesi, Mawasiliano ya Simu na Uchuuzi. Ni muhimu kasi ya ukuaji wa uchumi iendane na kiwango cha uwekaji akiba cha Taifa (National savings rates). Wakati uwekaji akiba Tanzania upo katika kiwango cha 16%, nadharia za uchumi zinaelekeza kuwa “Nchi zenye malengo ya kukua kwa

7% kwa mwaka inabidi ziwe na uwekaji wa akiba wa 35% ya pato la Taifa" (Pinto, 2014). Kwa uwekaji akiba nchini ni wa chini na duni, uhuru wa nchi unahatarishwa kwa kutegemea sana mitaji kutoka nje. Ili kuondokana na mrija huu wa mitaji ya nje, Chama cha Wazalendo kinataka kuhimiza uwekaji akiba kupitia mfumo wa hifadhi ya jamii ( Social Security Systems).

Licha ya Hifadhi ya Jamii kuwa ni kwa ajili ya pensheni, ACT-Wazalendo itatumia hifadhi ya jamii kama nyenzo (instrument) ya kukuza uwekaji akiba nchini ili kuweza kuwa na vyanzo vya mitaji ya uwekezaji wa ndani. Moja ya sababu kubwa ya kuwa na mporomoko wa thamani ya sarafu ya Tanzania ni nakisi ya uwekaji akiba maana 'nchi yenye nakisi ya akiba, sarafu yake hushuka thamani mpaka pale mali zake zinapokuwa rahisi sana kiwango cha kuvutia akiba za nje kuingizwa nchini'. Bila ya kuwa na uwekaji akiba mkubwa nchini, nchi yetu itakuwa kwenye mnyororo wa mitaji kutoka nje ambayo inahatarisha uhuru wa nchi yetu katika kuamua namna ya kuwekeza na maeneo gani ya kuwekeza.

Uwekezaji wa miradi mikubwa yenye faida kwa nchi kama miundombinu ya umwagiliaji, viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, barabara kuu, reli, bandari, viwanja vya ndege, vyuo vikuu na vyuo vya ufundi utafanywa na akiba kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kwani kwa uasili wake madai dhidi ya mifuko (liabilities) ni ya muda mrefu. Iwapo Watanzania milioni tano tu kati ya Watanzania milioni ishirini na mbili waliopo kwenye nguvu kazi wakiweka akiba ya shilingi thelathini elfu tu kwa mwezi (shilingi 20,000 itachangiwa na mwananchi na shilingi 10,000 na Serikali kwa kila mwananchi mchangiaji), akiba itakayowekwa itakuwa ni shilingi 1.8 trilioni kwa mwaka, sawa na 2.5% ya Pato la Taifa. Fedha hizi ni sawa na jumla ya Fedha zote Tanzania imeingiza kama Foreign Direct Investments kutoka nje mwaka 2013. Fedha hizi ni mtaji tosha kwa uwekezaji kwenye miradi ya muda mrefu na yenye kuweza kulipa vizuri na kufaidisha wanachama wa hifadhi ya jamii.

Kuna ugumu kwa watu masikini kujiwekea akiba kwa sababu ama ya kipato kiduchu

au kutokuwa na nidhamu ya kuweka akiba. Hata hivyo, watu masikini wengi katika nchi yetu ni wanachama wa vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) ili kuweza kufikia akiba yao wanapokuwa na mahitaji kama vile matibabu, elimu ya watoto wao na kupata mikopo ya gharama nafuu ili kuanzisha biashara ndogondogo. Mfumo wa Hifadhi ya Jamii utamwezesha masikini kuweka akiba kupitia vyama vyao vya hiari vya SACCOS na kupata mikopo nafuu ili kuongeza kipato chao. Muhimu kuliko yote mwanachama atapata Bima ya Afya na hivyo kuweza kupata matibabu bure bila ya kuathiri michango yake katika mfuko wa hifadhi ya Jamii. Hifadhi ya Jamii kwa wote itakuwa nguzo muhimu katika Sera za Chama cha ACT-Wazalendo na nyongeza muhimu sana katika kuhuisha Azimio la Arusha.

Katika kutekeleza Azimio la Arusha, Serikali ya wakati huo ilianza kampeni ya wananchi kuhamia kwenye vijiji vya ujamaa. Msukumo mkubwa pamoja na mambo mengine ulikuwa ni kuiwezesha Serikali kutoa huduma za kijamii kwa

urahisi. Vilevile wananchi walilima kwenye mashamba ya ujamaa kwa kutumia kauli mbiu nyingi ikiwemo kilimo cha bega kwa bega. Chama cha ACT- Wazalendo kitaka nataka Serikali kuwafuata wananchi huko walipo vijijini na kuwawezesha kulima mashamba yao binafsi wenyewe kwa tija kwa kupitia ushirika wa msingi ili kuongeza uzalishaji, kufungua viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo vijijini na kuunganisha uchumi wa vijijini na uchumi wa Taifa. **Ujamaa wa kidemokrasia unaosimamiwa na ACT-Wazalendo ni ujamaa wa kuzalisha na sio ujamaa wa kugawana tu.**

### *3.2.2 Kupambana na mfumo wa unyonyaji na ufisadi*

Hata uchumi ukue kwa kasi ya namna gani iwapo ukuaji huo unanufaisha kikundi kidogo cha watu hauna maana na ni hatari kwa uwepo wa taifa lenyewe. Ni lazima kuchukua maamuzi ya kujenga taasisi zenye nguvu ambazo zitaondoa hali hii ya uchumi kutajirisha wachache na kufukarisha wengi. Lazima kupambana na rushwa kwa vitendo na bila huruma wala kuoneana aibu.

Ufisadi utaondoshwa kwa kujenga mifumo madhubuti ya uwajibikaji na taasisi zake. Taasisi na mfumo utakaohakikisha kuwa watawala wanawajibika kwa umma kwa wanayoyatenda na wasiyoyatenda. Mfumo utakaohakikisha kuwa rasilimali za nchi zinarudi kwa wananchi ili kujenga miundombinu vijijini ikiwemo barabara, maji, nishati ya umeme na kuboresha huduma za kijamii hasa elimu na afya. Vinginevyo tutaendelea kuwa taifa vipande vipande kutokana na tofauti kubwa ya kipato na fursa ndani ya jamii. **ACT-Wazalendo tunasema Tanzania yenye watu fukara milioni thelathini na bilionea thelathini haikubaliki.**

Hapa nchini kwetu Tanzania, ufisadi unasukumwa na mambo makuu manne. Moja, ni rushwa ndogo ndogo zinazotokana na huduma mbovu za kijamii kama kwenye mahospitali, mashuleni na kwenye idara za Serikali kama polisi, mahakama na ardhi. Hizi hongo Mwalimu Nyerere alipata kuziita “little chai” ili kuharakisha huduma. Hongo za namna hii zinawaathiri sana wananchi masikini kabisa vijijini.

ACT WAZALENDO

Jambo la pili ni fedha zinazotumika kwenye siasa, ambapo vyama vya siasa hupewa fedha na matajiri ili kulinda maslahi yao. Hapa Tanzania tunashuhudia vyama vya siasa vikitumia vibaya ruzuku wanazopewa na Serikali lakini pia vikifadhiliwa fedha nyingi sana na matajiri ili kulinda matendo yao na haswa ukwepaji mkubwa wa kodi. Vyama vikishinda na kuunda dola vinaunda Serikali yenye sera zinazolinda matajiri hawa. Jambo la tatu ni makampuni makubwa ya kimataifa ambayo hutumia njia za kitaalamu kukwepa kodi na kutorosha fedha kwenda ughaibuni. Jambo la nne ni makundi ya kiharamia yanayojihusisha na madawa ya kulevya, ujangili na ujambazi. Kiasi fulani makundi haya huwa ni mtandao mmoja wenye lengo la kuhifadhi tabaka la Watawala na wenye nacho waendelee kunyonya wananchi.

Katika kupambana na ufisadi, hatuna budi ya kuvunja mfumo wa sasa unaokumbatia ufisadi. Mfumo wa siasa na uchumi tulionao sasa unazaa ubinafsi na hivyo ufisadi. Miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia minyukano ya wanasiasa dhidi ya rushwa, hata hivyo

hakuna chama hata kimoja cha siasa ambacho kinazungumzia kubomoa mfumo unaozaa ufisadi. ACT-Wazalendo inataka kujenga Ujamaa wa kiDemokrasia ambao unaojengwa juu ya misingi ya Azimio la Arusha na haswa Miiko ya Uongozi. Ni lazima kupiga marufuku viongozi wa kisiasa kujilimbikizia mali. Ni lazima kuwa wazi kabisa kuhusu maamuzi ya kisera yanayopelekea kubomoa mfumo uliopo sasa na kujenga mfumo mpya wa uchumi.

Masuala ya kiuchumi na hasa umasikini, afya, elimu na masuala ya rushwa ni mambo makuu ambayo Watanzania wanayaona kama changamoto kubwa zinazowakabili. Hivyo shabaha kubwa ya sera zitakazotekeleza Ujamaa wa kiDemokrasia ni kutokomeza umasikini na kuumilikisha uchumi kwa wananchi wenyewe.

### *3.2.3 Kilimo*

Ili kujenga uchumi shirikishi, ni muhimu kufanya jitihada za makusudi katika kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinaanza kuchangia vya kutosha katika ukuaji wa

uchumi. Shabaha ya muda wa kati katika sekta ya kilimo ni kuongeza Mapato ya fedha za kigeni kutokana na kilimo ikiwemo kilimo cha maua na mbogamboga hadi kufikia dola za kimarekani bilioni mbili kwa mwaka ifikapo mwaka 2025. Shabaha ya muda mrefu ni kujitosheleza kwa chakula na ziada kuuza nje na kuongoza katika nchi za Afrika Mashariki kwa kuuza nje Sukari na Mchele; Kurejea kuwa nchi ya kwanza duniani kwa kuuza nje Katani na bidhaa za Katani; Kuongoza Afrika kwa kuuza nje Korosho zilizokobolewa na Wakulima wote wa Tanzania kuwa na  hifadhi ya jamii.

**Chama cha ACT-Wazalendo kitaagiza serikali kuchukua hatua mahususi zifuatazo kuhusu kiilimo:**

1) Kilimo ndio shughuli kiongozi katika kutokomeza umasikini. Shughuli za Kilimo lazima ziendeshwe na wananchi wenyewe kwa kuwawezesha kumiliki ardhi, kuongeza tija na hivyo uzalishaji na kupata mitaji kwa kupitia mfumo wa hifadhi ya jamii.

2) Mfumo wa Hifadhi ya Jamii uwekewe utaratibu wa kuwepo kwa fao la Bei ya Mazao (Price Stabilization Benefit), Bima ya Mazao na Mifugo na mikopo ya gharama nafuu kwa vikundi vya wakulima ili kununua pembejeo za kilimo na ufugaji kwa lengo la kuhami mwananchi asitumbukie kwenye ufukara.

3) Ardhi na mashamba yote yaliyokuwa ya Mashirika ya Umma na kubinafsishwa yarejeshwe kwa wananchi wasio na ardhi kwa kuwagawia na kushiriki katika uzalishaji kwa kutumia mfumo wa 'outgrowers' scheme'.

ACT WAZALENDO

4) Mashamba makubwa ya kibiashara yatakapohitajika itakuwa ni jumla ya mashamba madogo madogo ya wananchi na pale uwekezaji utakapohitaji basi wananchi watamiliki theluthi mbili ya shamba husika na mwekezaji wa ndani au wa nje atamiliki theluthi moja tu.

5) Serikali itunge mfumo wa kodi unaoeleweka na usiotetereka (stable fiscal regime) katika sekta ya kilimo ili kuhakikisha kuwa mkulima anabakia na sehemu kubwa ya mapato yake.

6) Serikali iunde Mamlaka ya Kilimo ili kusimamia sekta ya kilimo. Wajibu wa kuhakikisha mazao ya kilimo ya wananchi yote yamenunuliwa kwa bei nzuri utakuwa wajibu wa Serikali kupitia Shirika la Umma litakaloundwa mahususi kwa kazi hiyo.

7) Dola kuhusika kikamilifu kwenye hifadhi ya mazao na kuanzisha mfumo wa soko kupitia soko la bidhaa (commodities exchange) ambao utashirikisha vyama vya wakulima na hivyo kufuta kabisa watu wa kati (middlemen).

8) Mfumo wa usambazaji wa pembejeo za kilimo utapaswa kurekebishwa ili kutoa nguvu kwa vyama vya msingi vya wakulima kununua pembejeo zao

wenyewe kwa wakati. Serikali itakuwa na wajibu wa usambazaji wa pembejeo kwa wakulima kupitia Shirika la Umma litakalokuwa na wajibu huo pekee.

### *3.2.4 Viwanda*

Shabaha ya muda wa kati ni kuhakikisha kuwa bidhaa za viwanda zinaliingizia Taifa mapato ya fedha za kigeni zaidi ya dola za kimarekani bilioni tatu kwa mwaka. Msukumo uwekwe kwenye bidhaa za nguo kwani zinaajiri watu wengi zaidi na mnyororo wake wa thamani ni mrefu mpaka kwa wakulima wa pamba nchini. Itakuwa ni marufuku kuuza nje malighafi (raw materials) isipokuwa kwa mazingira maalumu ikiwemo inapothibitika kuwa uwezo wa ndani wa nchi ni mdogo.

**Chama cha ACT-Wazalendo kitaagiza serikali kuchukua hatua mahususi zifuatazo kuhusu viwanda:**

1) Viwanda, vikiwemo vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi vipewe kipaumbele kikubwa

kwa kuwekewa vivutio vya kodi ikiwemo ruzuku za kufidia gharama za uzalishaji kama umeme (mfano viwanda vya kuzalisha sukari, saruji, ngozi, korosho na nyuzi za Pamba) na zawadi za kodi (exports tax credits) ili kuchochea mauzo ya nje.

2) Serikali ishiriki katika umiliki wa viwanda vya msingi kama vile viwanda vya chuma cha pua na kusimamia kikamilifu ushiriki wa sekta binafsi katika kuongeza uzalishaji viwandani.

3) Viwanda vya Tanzania vina fursa ya kuuza ndani ya Afrika Mashariki, Kati na Maziwa Makuu bidhaa kama unga, plastiki, saruji, sukari na vinywaji maradufu ya mauzo ya sasa. Hivyo serikali ihakikishe kwamba soko la kanda linakuwa ni kipaumbele cha kwanza katika uimarishaji wa viwanda.

### *3.2.5 Utalii*

Shabaha ya muda wa kati ni Tanzania iwe na uwezo wa kuingiza na kuhudumia watalii milioni 5 kwa mwaka na kuingiza mapato ya fedha za kigeni yasiyopungua dola za kimarekani bilioni 8 kwa mwaka. Makusudio ya Serikali katika sekta ya utalii isiwe ni kukusanya kodi tu bali iwe ni kuzalisha ajira na kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

Sekta ya utalii ina nafasi kubwa sana ya kuzalisha ajira kwa vijana na wananchi kwa ujumla. Pia mnyororo wa thamani wa sekta utalii ni mrefu na kwa kuwa nchi imejaaliwa vivutio vingi vya utalii inaweza kuleta fedha nyingi za kigeni kuweza kununua mashine na vipuri tusivyoweza kuzalisha wenyewe katika kipindi cha mpito. Thamani ya fedha za kigeni katika utalii lazima ziendane na thamani ya manunuzi yetu nje ya nchi na hasa mafuta ambayo yanatumia sehemu kubwa ya akiba yetu ya fedha za kigeni.

**Chama cha ACT-Wazalendo kitaagiza serikali kuchukua hatua mahususi zifuatazo kuhusu utalii:**

1) Kuweka mfumo rahisi wa kikodi katika sekta ikiwemo urahisi wa kupanua vyumba vya wageni vya mahoteli.

2) Utalii wa kitamaduni udumishwe ikiwemo kuboresha michezo kama riadha, mpira wa miguu, sanaa nk ili kutangaza nchi.

3) Shirika la ndege la taifa ni lazima liundwe upya na liwe chachu ya kuongeza mapato ya fedha za kigeni nchini.

4) Timu ya taifa ya mpira wa miguu itumike kutangaza nchi kwa kuwekewa lengo la kufika kombe la dunia kabla ya mwaka 2025 kwa kujenga shule za michezo katika kila mkoa wa Tanzania, Mashirika ya Umma kuwa na timu za michezo na mashindano ya michezo mashuleni kurejeshwa.

5) Sanaa kama vile nyimbo na filamu ziwe nyenzo za kutangaza nchi, kuongeza ajira kwa vijana kupitia vipaji vyao na kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

### *3.2.6 Madini, Mafuta na Gesi Asilia*

Sekta za Madini, Mafuta na Gesi Asilia ni sekta za maliasili ya nchi yetu. Sekta hizi zinaweza kuzalisha mapato ya kutosha ya Serikali ili kuboresha sekta nyingine kama vile Kilimo na uwekezaji katika Afya, Elimu na Hifadhi ya Jamii.

**Chama cha ACT-Wazalendo kitaielekeza serikali kuchochea mabadiliko makubwa katika sekta hizi za uvunaji wa maliasili ya nchi kwa kuchukua hatua zifuatazo:**

1) Maliasili zote za madini, mafuta na gesi asilia ziw mali ya wananchi KIKATIBA na uchimbaji wake lazima uwe na kibali cha wananchi (free prior informed consent).

2) Mfumo wa uchimbaji wa maliasili hizi ubadilike kutoka mfumo wa sasa wa kutoa leseni na kukusanya

kodi na mrahaba kwenda mfumo wa umiliki na ukandarasi. Mwekezaji awe mkandarasi, arejeshe gharama zake na faida iliyobakia kugawana na Serikali kwa makubaliano maalumu. Haki (Mineral Rights) iwe ya Shirika la Umma linalomilikiwa na Serikali na wananchi kwa asilimia 100. Wenye mitaji wawe wakandarasi wa Shirika hilo la Umma kwa mujibu wa mikataba (Revenue Sharing Agreements).

3) Mikataba yote ya uvunaji wa maliasili iwe wazi kwa wananchi. Mapato yatokanayo na mrahaba yagawiwe kwa maeneo yenye shughuli za uchimbaji kwa uwiano maalumu utakaowekwa. Mapato yatokanayo na mali asili ya nchi yawekwe kwenye mfumo maalumu na kutumika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, upanuzi wa huduma za afya na elimu, akiba kwa vizazi vijavyo na kuimarisha mfumo wa hifadhi ya jamii nchini.

ACT WAZALENDO

### *3.2.7 Hitimisho*

Sera za ACT-Wazalendo zinalenga kuelekeza nguvu kwenye uchumi na kujenga mazingira ya kufanya mageuzi makubwa (transformation) ya kiuchumi, kuwezesha kasi ya ukuaji uchumi kwa zaidi ya wastani wa asilimia 10 kwa muongo mzima na kujenga jamii ya watu walio sawa na huru. **Sekta msukumo za uzalishaji ni Kilimo, Viwanda, Usafiri wa kimataifa (transit trade) na Utalii. Sekta msukumo za matumizi/uwekezaji ni Elimu, Afya, miundombonu ya usafiri/usafirishaji na Hifadhi ya Jamii.**

Hata hivyo, yote haya hayatakuwa na maana iwapo mfumo wa fedha kupitia mabenki utakuwa umeshikwa na wageni. Nchi yetu haiwezi kuendelea iwapo mabenki makubwa yote yanamilikiwa na watu kutoka nje. Utaifishaji wa Mabenki uliofanyika mwaka 1967 na kuundwa kwa Benki ya Taifa ya Biashara, Benki ya Nyumba na Benki ya Maendeleo Vijijini ilikuwa ni maamuzi ya msingi sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Ubinafsishaji wa Benki ya Taifa ya Biashara na kufilisiwa kwa

Benki ya Nyumba ilikuwa ni maamuzi ya hovyo kabisa kupata kutokea katika nchi yetu.

Malengo ya kujenga uchumi shirikishi wenye uhuru mkubwa katika soko la mitaji hayawezi kufikiwa bila ya kuwa na Benki zinazomilikiwa na Watanzania wenyewe. Hivyo, Chama cha ACT-Wazalendo kitahimiza kuwa Benki ya Taifa ya Biashara irejeshwe kwenye mikono ya Watanzania kwa kumilikiwa na Serikali 50% na Wananchi na taasisi za wananchi kupitia soko la mitaji nusu iliyobakia. ACT-Wazalendo itahimiza pia Benki ya Maendeleo na Benki ya Kilimo kuwa na muundo wa umiliki kama wa Benki ya Taifa ya Biashara.

Mashirika yanayoendesha sekta nyeti katika uchumi kama Umeme, Reli, Bandari, Mkonga wa Taifa, Mafuta na Gesi Asilia, Bima ya Maisha, Benki ya Taifa ya Biashara, Madini ya msingi kama Chuma yataendeswa moja kwa moja na serikali na kwa ubia na wananchi, na kamwe hayatamilikishwa kwa wageni.

Shabaha yetu katika muda wa kati ni kuwa na Pato la Taifa la dola za kimarekani bilioni 90, uwekaji akiba usiopungua asilimia 30 ya Pato la Taifa na makusanyo ya kodi yasiyopungua asilimia 25 ya Pato la Taifa. **Tunalenga kuwa Tanzania itakuwa nchi ya 5 kwa ukubwa wa uchumi barani Afrika na ya kwanza katika Afrika Mashariki ifikapo mwaka 2030.**

ACT-Wazalendo tunataka kufufua utaifa wa Tanzania ili kila Mtanzania aone kuwa ana wajibu wa kujenga nchi yake kwa ajili ya leo na vizazi vijavyo. Tunataka kufufua uzalendo wa Taifa kwa kurejesha imani ya wananchi kwa viongozi wao kwa kutokomeza ufisadi kupitia Miiko ya Viongozi. Kujenga uchumi shirikishi wenye mfumo madhubuti wa uwajibikaji na unaowezesha kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi afanye kazi na kupata ujira unaotosha ni moja ya njia bora zaidi ya kujenga uzalendo miongoni mwa wananchi na viongozi wa Taifa hili. Tunataka Tanzania ambayo kila raia ana haki sawa ya kupata Elimu bora na Afya bora. Tunataka Tanzania ambayo kila raia ana Hifadhi ya

Jamii. Tunataka Tanzania yenye usawa. **Tunataka kujenga Taifa lenye kujitegemea kiuchumi na kiutamaduni, na ambalo linalinda na kudumisha usawa, ustawi wa jamii, uwajibikaji, demokrasia, na uongozi bora. Hii ndio ndoto yetu wana ACT - Wazalendo.**

# SEHEMU YA NNE

## 4.1 Miiko ya Uongozi

Ili kubomoa mfumo wa kinyonyaji na kifisadi, Chama cha Wazalendo (ACT-Wazalendo) kimeamua kurejesha miiko ya Uongozi na Kuiishi. Ni wazi kuwa kama chama tumejiwekea misingi mizito ambayo itahitaji kujitoa kikamilifu katika kuisimamia. Jukumu kubwa la usimamizi wa Itikadi, Falsafa na Misingi ya chama lipo mikononi mwa viongozi. Tunahitaji viongozi watakaojitoa kwa dhati kusimamia misingi hii. Hivyo basi, miiko hii ya uongozi imewekwa iwe dira ya viongozi wa ACT-Wazalendo na serikali itakayotokana nayo katika kuwatumikia wananchi.

### *4.1.1 Miiko ya viongozi*

1. Kiongozi wa ACT-Wazalendo au wa Serikali itokanayo na chama chetu au akiwa katika chombo chochote cha dola, katika Serikali za Mitaa na

Serikali Kuu sharti awe ni mtu mwenye shughuli halali inayompa kipato halali na asishiriki katika jambo lolote litakalomuweka katika mgongano wa kimaslahi unaompelekea yeye binafsi, familia yake, rafiki zake au jamii yake kufaidika kifedha au kwa namna nyingine.

2. Kiongozi sharti aweke wazi shughuli zake za biashara na nyakati zote akiwa kiongozi kwenye ofisi ya umma na awe haendeshi moja kwa moja shughuli hizo yeye mwenyewe.

3. Akiwa katika uongozi wa umma, kiongozi asiwe mkurugenzi katika kampuni yeyote binafsi au shirika la umma.

4. Kiongozi sharti aweke wazi vyanzo vyake vya mapato na mali zitokanazo kwa kuzingatia utaratibu wa sheria za nchi na Kanuni za Mwenendo na Maadili ya Viongozi wa ACT-Wazalendo na miongozo mingine ya chama.

5. Kiongozi asifanye biashara ya aina yeyote ile na chama na serikali itokanayo na ACT-Wazalendo wakati akiwa katika nafasi ya uongozi wa chama na/au serikali.

### *4.1.2 Tafsiri ya kiongozi*

Viongozi wanaotajwa hapa ni Viongozi wa Kitaifa wa chama, Rais, Mawaziri, Wabunge na Madiwani wanaotokana na ACT – Wazalendo. Kwa mujibu wa kifungu hiki kiongozi ni mtu peke yake, au mtu na mkewe au mke na mumewe.

ACT WAZALENDO

# NYONGEZA

Hotuba ya kiongozi wa chama Ndugu Zitto Ruyagwa Z. Kabwe aliyoitoa katika uzinduzi wa Chama cha ACT-Wazalendo siku ya Jumapili tarehe 29 Machi 2015 katika ukumbi wa Diamond Jubilee, Dar es Salaam

---

***Turejeshe nchi yetu Tanzania!***

Watanzania wenzangu, wageni waalikwa

Nawashukuru kwa kuwa pamoja nasi siku hii ya kihistoria.

Karibu Miaka 54 iliyopita tulipopata uhuru, Muasisi na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa kijana mwenye umri wa miaka 39, mwenye matumaini makubwa na taifa jipya na alikuwa na ndoto! Ndoto yake ilikuwa imejikita katika kuhakikisha taifa letu litakuwa taifa lisilo na umaskini, dhiki, ufukara; taifa lisilo na tofauti kubwa kati ya maskini na tajiri; taifa lenye usawa, haki na maendeleo,

ambapo watoto wote wanasoma shule bila kujali kipato cha mzazi; taifa ambalo wananchi wake wanamiliki uchumi wao.

Ndoto hii aliiamini kwa dhati na wananchi wote walikubali na kuota nae ndoto hii. Alilisimamia kwa maneno na vitendo kupitia Azimio la Arusha, sera zake na uongozi wake wa kizalendo. Mpaka mauti ilipomkuta aliamini katika misingi hii aliyojitahidi kuturithisha. Lakini miaka 16 baada ya kifo chake, ndoto yake imeyeyuka! Tulilonalo ni jinamizi alilolihofu Nyerere.

Leo hii:

*Watanzania wachache wameondoka katika unyonge na dhiki.*

*Watanzania wengi bado wapo katika hali ya dhiki.*

*Watanzania wachache wameshikilia uchumi: Warasimu, Wanasiasa na Matajiri wachache wenye mitaji.*

*Watanzania wengi bado kama Mwalimu Nyerere alivyosema "wananyonywa kiasi cha kutosha; wanapuuzwa kiasi cha kutosha".*

**Ndoto ya Mwalimu Nyerere bado haijawafikia wananchi.**

Sasa ndio wakati wa mabadiliko ya kimapinduzi.

Sasa ndio wakati wa kujenga Uchumi shirikishi ambao utaruhusu kila mwananchi kupata fursa ya kuboresha maisha yake. Sasa ndio wakati dola imara ipate nafasi ya kusimamia uchumi. Sasa ndio wakati kwa wananchi kuwa na uhuru wa kweli wa mawazo, fikra, kushirikiana na kuabudu. Sasa ndio wakati wananchi kuwa na nguvu ya kuwawajibisha viongozi wao. Sasa ndio wakati wetu watanzania kujirithisha upya nchi yetu!

Huu ndio wakati wa kubomoa uchumi wa kinyonyaji na kifisadi na kujenga uchumi wa wananchi. Haya ndio mabadiliko ya kimapinduzi tunayoyataka. Hii ndiyo ilikuwa ndoto ya Mwalimu Nyerere, na muda umefika wananchi turejeshe nchi mikononi mwetu!

Haya yamekuwa mawazo yangu kwa muda mrefu kwa sababu mimi ni zao la ndoto ya Mwalimu Nyerere. Nililelewa na mama yangu mzazi pekee mwenye ulemavu; nimeanza kusoma shule ya msingi nikiwa naenda peku. Lakini kutokana na kufaulu mitihani vizuri, sikuhitaji kuwa tajiri

kusoma mpaka Chuo Kikuu. Leo hii kutokana na elimu bora niliyoipata bure, nimesafiri na kufika katika nchi zaidi ya 70; nikiwa kama kiongozi nimekutana na kubadilishana mawazo na watu muhimu duniani kama vile wakuu wa nchi. Sio mimi peke yangu bali tupo maelfu tuliofaidika na mfumo huu. Lakini muhimu kupita yote, nimeweza kutumikia wananchi wa Kigoma na watanzania bungeni kwa miaka 10. Kama hii si ndoto iliyokuja kuwa kweli, ni nini?

Zitto Ruyagwa Z. Kabwe angezaliwa mwaka 2000, angekuwa kijana ambaye hajakamilisha elimu yake, haelewi lugha za kigeni kama kiingereza, hana ujuzi wowote na kama Mungu angeendelea kuninyima kipaji cha kuimba kama sasa ningeshindwa hata kutoka kama Diamond na Mwana FA! Mwalimu Nyerere asingepigania ndoto yake miaka ya 60 na 70, ningekuwa kama mamilioni ya vijana leo ambao wanahangaika kutafuta ajira na kipato bila ujuzi na elimu.

Na ndiyo maana siku ya leo ni muhimu kwangu. Nina furaha na heshima kubwa kuwa katika familia yangu mpya ya kisiasa. Familia inayoamini katika itikadi, misingi na tunu ninazoziamini.

Nimezungumza mara kadhaa kuhusu sababu za kujiunga na chama hiki. Chama cha Wazalendo ACT-Tanzania inaongozwa na misingi ya Uzalendo, Demokarsia, Uhuru wa fikra na matendo, Utu, Usawa, Uadilifu, Uwazi, Uwajibikaji na Umoja katika kila kitu. Chama hiki ni cha wananchi si wenyenchi wa sasa waliojimilikisha taifa. Chama hiki ni cha watanzania wote bila kujali kabila, dini, jinsia, rangi ya ngozi au hali ya ulemavu!

Tunapojadili wananchi kujimilikisha upya nchi yetu ni kupitia usimamizi wa sheria utakaohakikisha kuwa kuna uwazi na uwajibikaji wa viongozi. Uwazi tunaouamini ni ule utakaohakikisha kila mwananchi anapata taarifa za fedha zao, mikataba ambayo Serikali inaingia kwa niaba yao na taarifa za maslahi, mali na madeni ya viongozi wao. Tunataka uwazi katika uendeshaji wa Serikali na sisi tutaanza na uwazi katika uendeshaji wa chama chetu. Tunataka wananchi sio tu wajione kuwa sehemu ya uendeshaji wa nchi yao, bali pia wawe sehemu ya uendeshaji wa nchi yao.

Tunataka uwazi utakaoruhusu uhuru wa mawazo na uhuru wa wananchi kujieleza bila kuhofu

Serikali kuwachukulia hatua kwa kutoa mawazo yao. Ndio maana ACT-Wazalendo tunapinga vikali miswada ya sheria ambayo Serikali ya CCM imeiwasilisha bungeni katika mkutano unaoendelea. Miswada hii kama vile muswada wa Haki ya kupata taarifa, vyombo vya habari na ule wa makosa ya mtandao inalenga kuminya na kunyima haki za wananchi kuwasiliana kwa uhuru na kutoa mawazo yao kama inavyoainishwa katika katiba ya nchi.

Tunapojadili wananchi kurejesha taifa mikononi mwao tunazungumzia uwajibikaji. Ripoti ya Tume ya Marekebisho ya Katiba ilieleza moja ya sababu kubwa ya kushamiri rushwa, ufisadi na ubadhirifu nchini ni nanukuu **'kukosekana kwa mfumo madhubuti wa uwajibikaji'** nchini kwetu. Sababu kubwa ya ACT-Wazalendo kupinga Katiba inayopendekezwa ni kwamba, Katiba hiyo imechakachua nia hii ya kuweka mfumo wa uwajibikaji. Ndio maana tunawaambia wananchi waikatae Katiba hiyo kwa nguvu zao zote! Katiba inayoepndekezwa inastahili kadi nyekundu, tuikatae na kura ya hapana!

Iwapo wananchi hawawezi kuwawajibisha viongozi kwa matendo yao hatuwezi kujenga

jamii ya watu wanaoheshimiana na kutii sheria za nchi. Kila Mtanzania bila ya kujali cheo chake ni lazima awe chini ya sheria. Uwajibikaji ni lazima uanze na viongozi. Mnajua kuwa katika maisha yangu ya kisiasa hili ndio limekuwa jukwaa langu.

Kwa bahati mbaya tunaishi katika kipindi ambacho wanasiasa wengi wamekuwa wakikumbwa na kashfa mbalimbali za kifisadi na matokeo yake inajengwa picha kuwa kila mwanasiasa ni fisadi. Mfumo wa Uwajibikaji wenye uwazi utasaidia wananchi kutofautisha wanasiasa wanaosimamia maslahi ya umma na wale wanaosimamia maslahi yao binafsi na vyama vyao vya siasa. Mwungwana ni vitendo; nimewajibisha watu kwenye Buzwagi na mikataba ya madini, kwenye matumizi mabaya ya fedha za umma na juzi juzi kwenye akaunti ya Tegeta Escrow. Lakini matukio haya machache hayatoshi kujenga mfumo madhubuti wa Uwajibikaji. Ni lazima kufanya mapinduzi ya mfumo mzima wa uchumi wa nchi yetu na kujenga mfumo mpya unaohudumia kila Mtanzania na ambao kila Mtanzania anajivunia kuujenga. Hatuwezi kuwa Taifa linaloshikiliwa na vikundi vya wafanyabishara wachache na wanasiasa wanaofadhiliwa na wafanyabishara hao. ACT-Wazalendo inataka kujenga Taifa ambalo

viongozi wake wanawajibika kwa wananchi. Hii ndio fikra tunayotaka kurejesha. Hizi ndizo siasa zilizoasisi Taifa letu. Hatuna budi, ni lazima kurudi kwenye misingi na kuanza upya!

Kwa sababu ACT-Wazalendo imejikita kwenye misingi hii, tumelihuisha Azimio la Arusha. Sio tu tumeweka miiko ya uongozi lakini pia tumetunga kanuni za kutekeleza miiko hiyo na kuifanya kuwa sehemu ya Katiba ya chama chetu. Hitaji moja kubwa la Kanuni zetu za Maadili ni kutaka kila Kiongozi wa ACT-Wazalendo kuweka hadharani Maslahi yake, Mali na Madeni yake. Katika chama hiki huo ndio utamaduni wa kisiasa tunaotaka kuujenga. Kutenda tunachohubiri hata kabla ya kuingia kwenye uongozi wa Dola.

Chama cha ACT-Wazalendo kimeelekeza kikanuni kwamba kila Kiongozi wa chama lazima atangaze Mali zake na Madeni yake. Kila Kiongozi lazima aweke wazi maslahi yake ya kibiashara na mengineyo wazi ili kila anapotenda au kusema jambo wananchi wajue maslahi aliyonayo au la katika suala husika. Viongozi wote wa kitaifa wa ACT-Wazalendo watalazimika kufanya hivyo na kwa kuanzia leo hii mimi na Katibu Mkuu wetu tutaweka saini zetu mbele yenu kama mashahidi.

Naomba Mwanasheria wetu aje hapa tutekeleze matakwa haya ya kikanuni.

Fomu hizi zitakuwa kwenye tovuti ya chama ndani ya muda mfupi ujao ili kila mtanzania aone. Kila Kiongozi wa Chama ambaye Miiko ya Uongozi inamtaja anapaswa kuwa amejaza fomu hizi na kuziwasilisha kwa Katibu wa Kamati ya Uadilifu ifikapo tarehe 30 Juni 2015. Tunapopinga Viongozi wa Umma kufanya Biashara na Serikali na hivyo kuwa na mgongano wa kimaslahi na kushamiri kwa ufisadi, hivyo hivyo tunapinga Viongozi wa Chama chetu kufanya Biashara na Chama. Ni Marufuku Serikali kugeuzwa kuwa genge la watu wachache wanaopora rasilimali za Umma. Uadilifu tunaoutaka Serikalini ni lazima uanzie kwetu tunaohubiri.

Tutafanya haya kwa kubadilisha siasa zetu kuelekea kwenye masuala yanayowahusu wananchi; Wakulima, Wafanyakazi, Wafanyabiashara ndogo ndogo, Vijana, Wanawake na Wazee wetu. Tunataka kurejesha nchi yetu Tanzania kwa kujenga uchumi wa wote. Tunaporejea kwenye Azimio, hatusemi tunakwenda kutaifisha kila kitu na Serikali kuendesha shughuli zote za kiuchumi kama ilivyofanyika mwaka 1967 kwa

sababu za mazingira ya wakati huo. Tunaheshimu na kuthamini sekta binafsi na mchango wake katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo. Tunamaanisha kuwa ni lazima Dola isimamie uchumi. Sio kazi ya Serikali kufanya biashara. Lakini tunamaanisha kuwa ni lazima kurekebisha baadhi ya makosa yaliyofanyika kwenye ubinafsishaji na hususan ubinafsishaji holela uliofanyika kwenye sekta ya Kilimo na kupora ardhi ya wananchi wetu na kuwageuza kuwa manamba kwenye ardhi yao wenyewe.

Tunataka kutomokeza ukwepaji kodi. Tanzania inapoteza 15% ya makusanyo katika forodha kwa sababu ya ukwepaji wa kodi. Hii ni sawa na shilingi za kitanzania 490 bilioni kwa mwaka, fedha ambazo zingeweza kuchangia wananchi milioni 4 kwenye hifadhi ya Jamii. Tanzania inapoteza takribani shilingi 2 trilioni kila mwaka kwenye misamaha ya kodi. Hii ni fedha ambayo ingeweza kujenga reli mpya ya kati ya kisasa kutoka Dar mpaka Mwanza na Kigoma ndani ya miaka mitatu. Ili kuondoa upotevu huu ni lazima kupanua wigo wa kodi, kurahisisha kodi, kupunguza baadhi ya kodi kama vile kodi wanaotozwa wafanyakazi (PAYE) na kutumia teknolojia kuziba mianya ya ukwepaji wa kodi.

Aidha ni muhimu kuimarisha mfumo wetu wa kodi za kimataifa ili kuzuia utoroshaji mkubwa unaofanywa na makampuni ya kigeni. Ili tujitegemee kama Taifa ni lazima kukusanya mapato ya ndani ya kutosha. Ili kukusanya mapato ya ndani ya kutosha ni lazima kuweka mazingira mazuri ya biashara hasa kwa wafanyabishara ndogo ndogo kwani ndio wazalishaji wakubwa wa ajira.

***Kwa Vijana,*** Taifa hili ni lenu. Asilimia 75 ya Watanzania wapo chini ya miaka 40. Asilimia 65 ya wapiga kura wapo chini ya miaka 40. Nusu ya Watanzania ni watoto chini ya miaka 18. Kurejesha nchi kwenye misingi ni wajibu wa kujenga maisha yenu. Haikubaliki Vijana kuwa mzigo kwa wazazi kwa sababu tu uchumi hauzalishi ajira za kutosha. ACT-Wazalendo ndio jukwaa lenu la kufanya mapinduzi ya mfumo wa uchumi ili kujenga uchumi shirikishi unaozalisha ajira. ACT-Wazalendo inataka kuwajengea mfumo wa hifadhi ya jamii ambapo mtakapokuwa Wazee msipate tabu za pensheni na matibabu wanazopata wazee wetu hivi sasa. Shiriki kujijengea Taifa litakalohakikisha maisha yako ya sasa, baadae na ya kizazi kijacho.

***Kwa Wanawake,*** Ninyi ndio mhimili wa Taifa hili, wazalishaji wakuu na walezi wa Taifa letu. Kurejesha nchi kwenye misingi ni wajibu wa kutambua nafasi yenu stahili katika jamii. Nikiwa nimelelewa na Mwanamke mwenye ulemavu na mpiganaji wa kweli wa haki za wananchi walio pembezoni, sina namna kutoa heshima yangu zaidi ya kuongoza chama chenye misingi thabiti ya kumkomboa mwanamke. Msitarajie watu wengine kuwapigania mnapaswa kuchukua hatua kupitia jukwaa hili la ACT-Wazalendo.

***Kwa wafanyabishara,*** ninyi ndio mnachochea shughuli za Uchumi na kuzalisha ajira. Kuanzia kwa wamiliki wa maduka madogo mitaani mpaka kwa mameneja wa maduka makubwa; kutoka kwa wachuuzi na mama lishe mpaka kwa wamiliki wa viwanda na biashara; mnaamka kila siku asubuhi kujenga Taifa hili kwa kuzalisha mali na huduma. Baadhi yenu ambao mnamiliki viwanda, mashirika makubwa na kutoa ajira kwa maelfu ya wananchi, mmeanza mkiwa mnashona viatu na sare za shule, au mkitengeneza na kuuza mkate. Mmepata utajiri wenu na mali zenu kwa juhudi na jasho lenu na kutokana na fursa za kiuchumi zilizokuwepo kipindi hicho ambacho hakikuangalia dini, kabila, uwezo wa kifedha

au rangi ya ngozi. ACT-Wazalendo inataka kuwawekea mazingira bora ya biashara halali lakini pia kuhakikisha mnalipa kodi zenu na kutonyonya wafanyakazi wenu. Tunataka kuwawekea mfumo rahisi wa kodi, wenye kueleweka na unaowapa motisha kuzalisha zaidi ili kuongeza ajira zaidi na kupanua Pato la Taifa. Msipotimiza wajibu wenu biashara zenu hazitashamiri. Kurudi kwenye misingi ya Taifa hili ni kurejesha maadili katika biashara zenu.

***Kwa Wakulima,*** Wafugaji na Wavuvi, ninyi ndio mnaolilisha Taifa letu na kuleta fedha nyingi za kigeni kupitia mauzo nje. Kwa miongo mitatu sera za nchi zimewaweka pembeni na hivyo uchumi wenu kusinyaa. Viwanda vyote vya kusindika mazao yenu vimeuzwa kwa bei ya kutupwa licha ya kwamba jasho lenu ndio lilitumika kuvijenga. Miundombinu ya barabara, maji, umeme na mawasiliano haiwafikii ili muweze kupata masoko. Hamna hifadhi ya jamii wala bima ya mazao yenu. Ardhi yenu wamepewa wawekezaji na mnakodishiwa, mnapanga kwenye ardhi yenu wenyewe. Mmeachwa mkijihangaikia. Kurejesha nchi kwenye misingi kutawarudishia heshima yenu katika nchi yetu. ACT-Wazalendo ndio jukwaa sahihi kwenu kuhakikisha kuwa

tunajenga uchumi shirikishi ambao mtafaidika na jasho lenu. Hamna cha kupoteza isipokuwa minyororo ya kinyonyaji.

***Kwa Watanzania wote,*** mnaonisikiliza leo, katika ukumbi huu na popote mlipo kupitia vyombo vya habari, mnamo mwaka 1978 Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitangaza vita dhidi ya nduli Idi Amini na kusema: **"Tutampiga. Sababu za kumpiga tunazo. Nia tunayo. Uwezo wa kumpiga tunao".**

Tanzania ipo katika vita hivi sasa: Vita dhidi ya Ufisadi; Vita dhidi ya uporaji wa rasilimali zetu ; Vita dhidi ya Siasa chafu ; Vita dhidi ya Uchumi wa kinyonyaji. Vita dhidi ya kuporomoka kwa Utaifa wetu.

Tunapaswa kufanya jambo moja tu, nalo ni kupigana vita hizi. Ni vita kwa ajili ya kurejesha ndoto tuliyoota miaka 54 iliyopita na Muasisi wetu Mwalimu Julius Nyerere. Tunataka kurejesha nchi kwa wananchi, tunataka kujimilikisha nchi yetu. Wananchi wawe WENYE nchi! Tutimize ndoto yetu ya kuona;

Tanzania yenye Dola madhubuti,

Tanzania yenye Wananchi wenye mwamko,

Tanzania yenye sekta binafsi iliyochangamka,

Tanzania yenye uchumi unaonufaisha watu wote.

**Sababu tunazo. Nia tunayo. Uwezo tunao.** Twendeni tukajenge Chama kitakachorejesha misingi ya Taifa letu.

Asanteni sana

